Tanzania kuelekea 2015

Maoni na matakwa ya wananchi juu ya uongozi wa kisiasa

1. Utangulizi

Uchaguzi ni kiwango cha juu cha uwajibikaji wa kisiasa. Unatoa fursa kwa wapiga kura kuwaondoa viongozi wasiowajibika au kuwapa nafasi nyingine ya kuwajibika. Pia, unatoa nafasi adimu kwa wapiga kura kufanya maoni yao yasikilizwe. Uchaguzi mkuu ujao nchini Tanzania utafanyika mwaka 2015. Rais mpya atachaguliwa, pamoja na mamia ya wabunge. Mamia ya wanasiasa watatumia miezi kadhaa kufanya kampeni, kujaribu kuwashawishi wananchi kuwachagua.

Lakini ni masuala gani yaliyo muhimu zaidi kwa wapiga kura wa Tanzania? Wanavionaje viwango vya utendaji kazi wa viongozi wao? Je, wabunge wanatekeleza ahadi zao walizotoa uchaguzi mkuu uliopita? Na je, wapiga kura watawachagua tena wabunge hao? Ni chama gani cha siasa na wanasiasa kinachokubalika au kutokukubalika na wananchi wengi? Wananchi wanamtaka nani kuwa Rais wao ajaye? Na je, kuna mwenendo wa muda mrefu wa matakwa ya wapiga kura?

Majibu ya maswali haya ya kimsingi yanakosekana kwenye vichwa vya habari vya magazeti na ripoti nyingi. Katika muhtasari huu, Twaweza kupitia Sauti za Wananchi, utafiti wa kwanza Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu za mkononi, unawasilisha mambo tisa kuhusu matakwa na upendeleo wa wananchi kwa kutumia takwimu za hivi karibuni. Matokeo yametokana na awamu ya 24 ya utafiti wa *Sauti za Wananchi* uliofanyika mwezi Septemba 2014 (wahojiwa 1445) (www.twaweza.org/sauti). Takwimu hizi zimelinganishwa na zile za miaka miwili iliyopita kutokana na utafiti wa msingi wa *Sauti za Wananchi* uliofanyika mwezi Oktoba-Desemba 2012 (wahojiwa 2,000) na utafiti wa awamu ya 10 uliofanyika mwezi Oktoba 2013 (wahojiwa 1574).

Muhtasari huu umeandaliwa na Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania. Wachangiaji ni Elvis Mushi, Youdi Schipper, Evarist Kamwaga, Tunu Yongolo na Rakesh Rajani.
Takwimu zilikusanywa na Ipsos Tanzania. Imetolewa Novemba 2014.

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | barua pepe: uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Matokeo muhimu ni:

- Watanzania wanasema changamoto za kiuchumi, afya na elimu ni matatizo makubwa zaidi yanayoikabili nchi yetu
- Wapiga kura wanakumbuka ahadi za Wabunge wao, ambazo nyingi hazijatekelezwa.
- Viwango vya kukubalika kwa viongozi wa kisiasa vimepungua kwa vyama vyote
- Uungwaji mkono CCM unashuka lakini chama kina dhidi ya wapinzani wake wa karibu, Chadema na CUF
- Hakuna mgombea urais anayeongoza, uwanja wa ushindani bado wazi

2. Mambo tisa kuhusu wapiga kura, masuala na wawakilishi

Jambo la 1: Changamoto za kiuchumi, afya na elimu ni matatizo makuu nchini

Walipoulizwa ni matatizo yapi matatu makubwa yanayoikabili Tanzania, wananchi walieleza kuwa umaskini, afya na elimu ni matatizo makubwa zaidi yaliyotajwa mwaka 2014, na kwamba matatizo haya yameshika nafasi ya juu kitaifa kwa miaka mitatu mfululizo (Kielezo cha 1). Ukiangalia mwenendo wake, idadi ya watu waliotaja umaskini kama tatizo kubwa linalowakabili imeongezeka zaidi kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Watu kwa kiasi fulani hawaoni tatizo sana kuhusu elimu ndani ya mwaka huu wa 2014 kuliko ilivyokuwa mwaka 2013. Umma kwa ujumla, hasa vyombo vya habari, vilitawaliwa na taarifa/habari kuhusu masuala ya ubora wa elimu katika mwaka 2013, hali ambayo ni tofauti mwaka 2014. Hii inaweza kuwa sababu ya kupungua kwa wananchi waliotaja elimu kama tatizo. Mchakato wa mabadiliko ya Katiba ulitajwa kama tatizo linaloikabili nchi ndani ya mwaka huu wa 2014, pale ambapo mambo mengi yaliandikwa kuhusu uandikaji wa rasimu ya Katiba.

Kielelezo cha 1: Je, ni matatizo gani matatu makubwa zaidi yanayoikabili Tanzania leo? (asilimia ya majibu yanayoonesha tatizo)



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi,* Utafiti wa Awali (Oktoba – Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na awamu ya 24 (Septemba 2014)

Jambo la 2: Kiwango cha kukubalika kwa utendaji kazi wa viongozi wa kisiasa kinashuka

Wananchi waliulizwa wanavyoona kiwango cha utendaji kazi kwa ujumla wa viongozi mbalimbali wa kisiasa – viongozi wa kuchaguliwa na wale wa kuteuliwa. Katika makundi yote ya viongozi (asilimia inayoona utendaji kazi mzuri) wananchi wanaona kiwango cha utendaji kazi wa viongozi kiko chini na kimekuwa kikishuka tangu mwaka 2012 (Kielelezo cha 2).

Kiwango kimeshuka zaidi kuanzia mwaka 2012 hadi 2014 hasa kwa wenyeviti wa vijiji/mitaa na madiwani, ambapo kiwango kwa wenyeviti, kimeshuka kwa 25% na madiwani kwa 23%.

Kielelezo cha 2: Kiwango cha utendaji kazi wa viongozi waliochaguliwa nchini (asilimia ya wanaoona kiwango ni kizuri)



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi,* Utafiti wa Awali (Oktoba – Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na awamu ya 24 (Septemba 2014)

Jambo la 3: Wabunge wanatoa ahadi nyingi, lakini hawazitekelezi

Uchaguzi mkuu uliopita ulifanyika mwaka 2010, wabunge 239 walichaguliwa kuwakilisha maslahi ya wapiga kura wao. Wakati wa kampeni za uchaguzi, wabunge walifanya kampeni ili kupata kura, na mara nyingi walitoa ahadi nyingi kwa wapiga kura. Kama kielelezo 3A kinavyoonesha, karibu wapiga kura 8 kati ya 10 (79%) bado wanakumbuka ahadi zilizotolewa na wabunge wao wakati wa kampeni.

Kielelezo 3B kinaonesha kuwa ahadi nyingi walizotoa wagombea kwa wapiga kura zilihusu miradi ya ujenzi: kujenga au kukarabati barabara (77%), kujenga au kuboresha vyanzo vya maji (64%), ujenzi wa hospitali (38%) na ujenzi wa madarasa zaidi kwenye majimbo yao (23%). Ahadi hizi kwa ujumla ziliendana na mambo yaliyobainishwa na wananchi kama matatizo yaliyokuwa yanaikabili nchi yetu (angalia jambo la 1). Hii ilionesha kuwa, wanasiasa wanajua wanachohitaji wapiga kura wao.

Kwa bahati mbaya, ni mwananchi 1 tu kati ya 8 (12%) aliyeripoti kuwa mbunge wake ametekeleza ahadi zake zote, kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 3C. Wananchi 54% walisema wabunge wao walikuwa wametekeleza baadhi tu ya ahadi zao, wakati wananchi 32% walisema wabunge wao hawakutekeleza ahadi hata moja. Hata hivyo, kama inavyoonekana kwenye 3D, wananchi wanatekeleza sehemu tu ya wajibu wao, ikiwa wananchi wanne kati ya kumi (38%) wakiwa wameripoti kuwa wao wenyewe au jamaa zao ndani ya jamii wamefuatilia utekelezaji wa ahadi hizo kwa mbunge wao.

Kielelezo 3A: Je, unafahamu ahadi alizotoa mbunge wako?



Kielelezo 3B: Ahadi 10 kubwa zilizotolewa na wabunge



Kielelezo 3C: Je, mbunge wako alitekeleza ahadi alizotoa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2010?



Kielelezo 3D: Je, wewe au mtu yeyote kutoka jamii yako alifuatilia ahadi alizotoa mbunge wako?



Source of data: *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 24 (Septemba 2014)

Jambo la 4: Karibu nusu ya wabunge wote (47%) wana hatari ya kubwagwa uchaguzi ujao

Uchaguzi mkuu ujao unatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka 2015. Watanzania nane kati ya kumi wanaripoti kuwa wanafahamu majina na vyama vya wabunge wao (takwimu hazijaoneshwa).

Walipoulizwa kama watampigia tena kura mbunge wao wa sasa, karibu nusu ya Watanzania wote (47%) walisema hapana - tazama Kielelezo cha 4. Wahojiwa waliosema wasingempigia kura mbunge wao, ni wale walioripoti pia kuwa mbunge wao ametekeleza aidha ahadi chache au hajatekeleza ahadi yoyote aliyotoa katika uchaguzi uliopita.

Kielelezo cha 4: Je, unafikiria kumchagua tena mbunge wako?



Source of data: *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 24 (Septemba 2014)

Sauti za Wananchi iliuliza kuhusu sifa za wanaogombea ubunge. Watu watatu kati ya wanne (74%) walitaja kuwa wangeangalia kiwango cha elimu ya mgombea (Kielelezo cha 5). Nusu ya wahojiwa hao wanatarajia mbunge awe na angalau elimu ya shahada/digrii (takwimu hazijaoneshwa). Umri wa mgombea pia ilitajwa kama jambo la pili muhimu katika sifa za mgombea, kuzidi hata kuonekana mwaminifu, mnyoofu, mkweli, au muadilifu. Kati ya wale waliosema wanaangalia umri, walifikiri kuwa mbunge anapaswa kuwa na umri wa miaka 40 au zaidi (takwimu hazijaoneshwa).

Kielelezo cha 5: Sifa muhimu za mbunge



Source of data: *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 24 (Septemba 2014)

Jambo la 5: CCM ina nafasi ya kushinda 2015, lakini kwa asilimia ndogo

Kwenye uchaguzi mkuu uliopita, vyama vya siasa vilitumia msemo wa “mafiga matatu”. Kauli hii ya hamasa, iliwataka wapiga kura kuwachagua wagombea kutoka chama kimoja katika nafasi ya urais, ubunge na udiwani. *Sauti za Wananchi* iliuliza upendeleo wa wapiga kura katika kila uchaguzi, vile vile iliwauliza chama wanachokipendelea. Matokeo katika Kielelezo cha 6 yanaonesha kuwa upenzi wa chama haubadiliki kwenye aina tatu za wagombea wa uchaguzi.

Takwimu kimsingi zinaonesha dondoo muhimu tatu. Kwanza, mwaka 2014 CCM inaendelea kuongoza dhidi ya upinzani kwenye uchaguzi wa ngazi zote tatu. Hususan, ushindi huo unaonekana kwenye uchaguzi wa Rais kwa mujibu wa matokeo haya: takwimu zinaonesha kuwa kama uchaguzi ungefanyika mwezi Septemba 2014, CCM ingeshinda uchaguzi hata kama vyama vyote vya upinzani vingeungana na kuweka mgombea mmoja wa urais, hata kama wote wanaopigia kura mgombea badala ya chama wangempiga kura huyo mgombea.

Pili, CCM inapoteza sehemu ya kura - lakini kura za Chadema pia zinapungua, ambacho ni mshindani mkuu wa CCM Tanzania Bara. Kati ya mwaka 2012 na 2014, vyama vyote viwili vimepungukiwa kura kwa mujibu wa takwimu za ubunge kwenye kielelezo B: Kura za CCM zimepungua kutoka asilimia 60 hadi 46, Chadema kutoka asilimia 31 hadi 24. Hii ina maana kuwa, vyama vyote viwili vinakabiliwa na kupungua kwa kura kwa takriban robo ya asilimia ya kura zao za mwaka 2012.

Tatu, kupungua kwa sehemu ya kura kwa pande zote mbili zinazoongoza kunawiana na ongezeko la asilimia ya wananchi ambao wana nia ya kupiga kura kuchagua wagombea binafsi, badala ya wagombea wenye vyama. Sehemu ya wapiga kura waliosema “sitapigia vyama bali wagombea” imepanda kutoka asilimia karibu sifuri mwaka 2012 hadi asilimia 17% kwa ngazi zote tatu za uchaguzi kwa mwaka 2013 na 2014. Wakati huo huo, wananchii wameripoti kuwa hawana vyama, tofuati na kipindi cha nyuma: wasio na vyama walikuwa 0% mwaka 2012 na sasa ni 10% mwaka 2014 (kielelezo D).

Kielelezo cha 6: Kama uchaguzi ungefanyika leo, mgombea wa chama gani ungempigia kura?



Kielelezo B: Mbunge



Kielelezo C: Diwani



Kielelezo D: Upenzi wa chama



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi,* Utafiti wa Awali (Oktoba – Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na awamu ya 24 (Septemba 2014)

Jambo la 6: Mwenendo wa upigaji kura wa Rais kwa chama tawala ukoje?

Je, kuna matarajio gani ya muda mrefu kwa chama tawala? Kielelezo cha 7 kinaonesha mwenendo wa upigaji kura wa kumchagua Rais. Takwimu za matokeo zimechanganywa kutoka chaguzi tatu zilizopita na awamu tatu za takwimu za utafiti wa *Sauti za Wananchi* kuhusu uchaguzi wa kisiasa. Wakati takwimu za upigaji kura zinaonyesha kushuka kwa sehemu ya kura za CCM mwaka 2013, takwimu za hivi karibuni zaidi zinaonyesha kuongezeka uungwaji mkono kwa chama tawala.

Kielelezo cha 7: Mwenendo wa kura za CCM kwenye uchaguzi wa Urais na matokeo ya upigaji kura ya hivi karibuni



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi,* Utafiti wa Awali (Oktoba – Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na awamu ya 24 (Septemba 2014)

Kielelezo 8 kinaonesha idadi ya wananchi wanaojihusisha na vyama kwa makundi ya umri. Takwimu zinaonesha Chadema inaungwa mkono zaidi na makundi ya vijana (chini ya miaka 35), wakati asilimia kubwa ya wapiga kura walio na umri wa utu uzima (miaka 35 na zaidi) wanaunga mkono CCM. Aidha, asilimia kubwa ya wapiga kura vijana hawajihusishi na chama chochote cha kisiasa. Mtawanyiko huu wa uhusiano wa chama kwa makundi ya umri - kama utabaki ulivyo kwa kipindi kirefu - utatoa "faida za kidemografia" kwa upinzani hapo baadaye, hasa kwa sababu ya ongezeko la kasi la idadi ya watu.

Kielelezo cha 8: Upenzi wa chama, kwa makundi ya umri



Source of data: *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 24 (Septemba 2014)

Jambo la 7: Ushindani wa kupata mgombea wa CCM ni mkubwa sana

Kwa kipindi chote cha mwaka jana, shinikizo lilikuwa likiongezeka ndani ya chama tawala CCM, kuhusu nani atakuwa mgombea Rais wa chama hicho mwaka 2015. Kanuni za chama tawala zinakataza wagombea kujitokeza na kutangaza rasmi kugombea urais mpaka chama kiwaruhusu kufanya hivyo. Hata hivyo, watu kadhaa wanaotaka kugombea urais wametangaza nia yao ya kugombea urais.

Wahojiwa waliojitambulisha kuwa ni wanachama wa CCM waliulizwa ni nani anapaswa kupeperusha bendera ya CCM kwenye uchaguzi ujao? Kundi kubwa (42%) mwaka 2012 walisema hawana uhakika, lakini idadi hiyo imepungua hadi 18% mwaka 2014, angalia Kielelezo cha 9. Baadhi ya wahojiwa (24%) hawakutaja jina lolote lakini walieleza kuwa watamuunga mkono mgombea ambaye atapendekezwa na chama.

Kati ya wale waliotaja majina ya watu wanaowataka, asimilia 17 Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, akifuatiwa na Waziri Mkuu wa sasa, Mizengo Pinda (14%). Lowassa ameonekana kumzidi Pinda mwaka huu tofauti na ilivyokuwa mwaka 2012. Takwimu hizi zinaweza kutokana

na ukubwa wa jina la Waziri Mkuu, ikiwa Waziri Mkuu ana jukumu muhimu kama kiongozi wa kitaifa na kiongozi wa Serikali Bungeni anayejitokeza mara kwa mara kwenye vyombo vya habari. Hakuna mgombea mwingine aliyepata zaidi ya 10% mwaka 2014. Sehemu kubwa (24%) imekwenda kwa 'mtu yeyote atakayeteuliwa na CCM' na waliosema 'sina uhakika' ni asimilia 18. Hii ina maana kuwa pengine chaguo halisi litatokana na michakato ya ndani ya CCM, badala ya maoni ya mgombea.

Kielelezo cha 9: Nani unafikiri anafaa kuwa mgombea wa CCM uchaguzi ujao?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi,* Utafiti wa Awali (Oktoba – Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na awamu ya 24 (Septemba 2014)

Jambo la 8: Umoja wa vyama vya siasa una nafasi katika uchaguzi ujao

Wakati wa vikao vya Bunge, vyama kadhaa vya siasa vya upinzani viliunda umoja wenye jina la Ukawa (Umoja wa Katiba ya Wananchi). Ukawa imeundwa na CUF, Chadema na NCCR Mageuzi na baadhi ya wajumbe 201 wa Bunge Maalum la Katiba. Hivi karibuni, vyama hivyo chini ya Ukawa vilitangaza kuwa vitaweka mgombea mmoja kwenye uchaguzi wa Rais na nafasi nyingine muhimu.

Ili kupima uwezekano wa ushindi kwa umoja wa vyama vya upinzani, ***Sauti za Wananchi*** iliuliza swali lifuatalo: "Katika uchaguzi wa Rais ujao mwaka 2015, chukulia tuna mgombea mmoja wa upinzani, wewe ungemchagua nani?". Kielelezo cha 10 kinaonesha kuwa (Septemba 2014) karibu nusu (47%) ya wahojiwa wangeichagua CCM wakati karibu theluthi moja wangempigia kura mgombea wa umoja wa vyama vya upinzani.

Nani atashinda uchaguzi ujao wa Rais? kwa sehemu itaamriwa na wapiga kura "ambao wanapigia mtu": yaani, watu waliosema wao watampigia mgombea na siyo chama. Kura za kundi hili zitategemea ubora wa wagombea. Kama kura hizo zikigawanywa kwa CCM na upinzani, CCM itashinda urais kwa kuzidi upinzani kwa kura nyingi kiasi. Kutakuwa na kitisho kwa ushindi wa CCM kama wapiga kura wote wanaomchagua mtu badala ya chama watapigia kura mgombea wa umoja wa upinzani, kitu ambacho kina uwezekano mdogo kutokea, isipokuwa kama kutafanyika mbinu mpya za ushawishi kwa wapiga kura.

Kielelezo cha 10: Kwenye uchaguzi wa Urais ujao mwaka 2015, chukulia tuna mgombea mmoja wa Urais wa vyama vya upinzani, utamchagua nani? (2014)



Source of data: *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi-awamu ya 24 (Septemba 2014)

Kundi lililosema kuwa wangemchagua mgombea wa umoja wa upinzani lilipoulizwa kuwa nani anapaswa kuwa mgombea urais, watu 4 kati ya 10 (41%) walimtaja Wilbrod Slaa (Chadema). Majina mengine ya viongozi wa upinzani yaliyopata zaidi ya 10% yalikuwa: Ibrahim Lipumba (14%) wa CUF na Freeman Mbowe (11%) wa Chadema (Kielelezo cha 11).

Kielelezo cha 11: Ikitokea upinzani umeungana kuwa kundi la vyama, nani wamteue kuwa mgombea urais?



Source of data: *Sauti za Wananchi,* Baseline Survey Awamu ya 24 (Septemba 2014)

Jambo la 9: Ushindani wa urais bado uko wazi

Katiba ya sasa ya Tanzania inaruhusu Rais kushika madaraka kwa awamu mbili tu. Hii ina maana kuwa, mwisho wa awamu ya pili ya Rais Jakaya Kikwete itakuwa 2015, na atapaswa kuandaa njia kwa ajili ya Rais mpya.

Wahojiwa waliulizwa swali lifuatalo: Kama uchaguzi wa Rais ungefanyika leo, ungemchagua nani kama mtu huyo angekuwa mgombea? Mwaka 2014, takwimu za kisiasa zinaonesha mwenye asilimia za juu ni Edward Lowassa (13%) wa CCM, Mizengo Pinda (12%) wa CCM na Wilbrod Slaa wa Chadema (11%). Viongozi wengine wa kisiasa waliotajwa na zaidi ya 5% ya wahojiwa wa mwaka 2014 walikuwa ni Ibrahim Lipumba (6%) wa CUF na Bernard Membe (5%) wa CCM (Kielelezo cha 12).

Hata hivyo, kama ilivyokuwa huko nyuma, sehemu kubwa ya majibu ya wahojiwa ilikuwa ni "sijui". Mtu mmoja kati ya wapiga kura watatu (33%) alijibu kuwa hakujua (Kielelezo cha12), idadi ambayo ni karibu sawa na jumla ya asilimia za wagombea watatu wenye alama za juu zikichanganywa pamoja. Hii inaonesha kuwa kinyang'anyiro cha urais kiko wazi zaidi, kwa maana kwamba Watanzania bado hawajashawishika wa kutosha na wagombea waliojitangaza. Kwa maana hiyo, upenzi wa chama, kama inavyooneshwa kwenye jambo la 5, una uwezekano wa kuchangia sana kuamua nani mshindi. Uwanja wa ushindani unaweza kuwa mpana zaidi endapo mgombea muhimu wa CCM atajiondoa kwenye chama na kujiunga na upinzani.

Kielelezo cha 12: Mbali na Rais Kikwete, kama uchaguzi wa Rais ungefanyika leo, ungemchagua nani kama mtu huyo angegombea?



Source of data: *Sauti za Wananchi,* Utafiti wa Awali (Oktoba –Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na awamu ya 24 (Septemba 2014)

3. Hitimisho

Matokeo haya kutoka Septemba 2014 yanaonesha kuwa CCM inaendelea kuungwa mkono na wananchi wengi Tanzania Bara. Hata hivyo, haivizidi sana vyama vingine vya siasa kama ilivyokuwa huko nyuma, lakini bado CCM ni chama maarufu zaidi katika nyanja mbalimbali, ikiwa ni pamoja kuwa na wanachama wengi (54%) dhidi ya 27% ya mpinzani wake mkuu Chadema na nafasi kwenye uchaguzi wa Rais (54%) dhidi ya 23% ya Chadema.

Muhtasari pia unaonesha kuwa hakuna kigogo wa kisiasa ndani ya CCM ambaye ana ushindi wa wazi kama mgombea urais kwa mwaka 2015. Vile vile, umeonesha kuwa hakuna mgombea urais kutoka chama chochote ambaye ana uhakika wa kuongoza. Hii ilijitokeza tulipouliza swali la kutaja majina ya wagombea.

Jambo linaloonekana kwa sasa ni kuongezeka kwa kundi la wapiga kura ambao hawajaamua wampigie nani kura, kundi ambalo ni kubwa kuliko idadi ya wafuasi wa mgombea yoyote. Hii inaonesha kuwa Watanzania bado hawajaamua wamchague nani au hawajashawishiwa vya kutosha na mgombea yeyote kati ya wagombea wanaoongoza, na hivyo, mgombea yeyote miongoni mwa waliojitangaza au atakayeibuka mpya ambaye atawavutia na kuwashawishi kikamilifu wapiga kura anaweza kushinda. Mwelekeo wa upigajikura unaonekana kufuata upenzi wa vyama. Kwa hiyo, swali gumu hapa ni iwapo haiba ya mgombea itashinda upenzi wa chama; uchaguzi utakuwa mgumu na hautabiriki.

Sauti za Wananchi ilibainisha pia masuala ambayo Watanzania wanayaona kuwa matatizo makubwa yanayoikabili nchi. Matatizo hayo ni umaskini, afya, elimu na maji. Hii inaashiria kuwa wagombea urais wanaweza kupata nguvu za kuwashawishi wapiga kura kwa kujiuliza watafanya nini kutatua matatizo haya, na ni jinsi gani wanaweza kuwasilisha mawazo yao yenye ufumbuzi ambayo yatawashawishi wapiga kura.

Takwimu pia zinaonesha kuwa wapiga kura wanafahamu kuwa wagombea wa kisiasa mara nyingi hutoa ahadi ambazo wanashindwa kuzitekeleza. Kwa wagombea watarajiwa, hii ni ishara tosha kuwa wapiga kura hawataamini kiurahisi ahadi zinazotolewa wakati wa kampeni za mwaka 2015. Wanasiasa katika kila ngazi lazima wapewe changamoto ya kuja na ahadi muhimu za kisera zilizo wazi, zinazopimika na kuaminika ambazo wananchi watazitumia kama kipimo cha matokeo ya utendaji kazi wao na kama mafanikio yao.

Uchaguzi wa mwaka 2015 una uwezekano wa kuwa moja kati ya uchaguzi mgumu na wenye ushindani mkali katika historia ya Tanzania, kwenye ngazi zote, urais na ubunge. Wagombea wanahitaji kufanya kazi kubwa ili kupata kura. Vivyo hivyo, wapiga kura wana nafasi nzuri zaidi ya kuhakikisha sauti zao zinasikika kuliko hapo nyuma. Jambo la kujiuliza ni iwapo mjadala na maslahi ya umma na masuala muhimu ya wananchi yataongoza upigaji kura badala ya haiba ya wagombea na vishawishi haramu kama vile rushwa na hongo.

Maelezo kuhusu mbinu ya utafiti

Sauti za Wananchi ni utafiti wa kimakundi unaofanyika Tanzania Bara (Zanzibar haimo kwenye utafiti huu) wenye uwakilishi wa kitaifa na hufanywa kwa njia ya simu za mkononi. Kanuni ya msingi ya muundo wa utafiti huu ni sawa na utafiti uliozoeleka wa mahojiano ya ana kwa ana. Makundi mawili ya wahojiwa hubainishwa ambayo ni wahojiwa kutoka mijini na pia vijijini. Sampuli ya kaya 2,000 zilitengenezwa kupitia hatua tatu, kwa kutumia uchaguzi nasibu kila hatua: kwanza, maeneo ya kuhesabia 200 yalichaguliwa kinasibu, kisha kaya 10 zichaguliwa kinasibu kutoka kwenye orodha ya kaya zote katika kila Eneo la Kuhesabia (enumeration areas), na kisha mtu mzima mmoja alichaguliwa kinasibu katika kila kaya.

Kila kaya ilipatiwa simu ya mkononi na sinia (chaja) inayotumia nishati ya jua. Wakala wa kituo cha kupigia simu huwasiliana na kila kaya kila mwezi na kuwauliza maswali yanayohusu mada na masuala mbalimbali. Kaya na sifa za wahojiwa hutumika kuchambua makadirio ya utafiti kwa masuala yasiyo na majibu kwa kusawazisha mizani ya wahojiwa, ambao ni utaratibu wa viwango vya kitakwimu kwenye tafiti za makundi ya wahojiwa. Kwa taarifa zaidi tembelea www.twaweza.org/sauti